NIH Fogarty International Center

# Kituo cha Kimataifa cha Fogarty katika NIH kinaendeleza sayansi kwa afya ya kiulimwengu



*Picha kwa hisani ya Neerja Vashist*

Matamanio ya kuwa huru na magonjwa - kuwa na afya - kunatuunganisha sote. Kituo cha Kimataifa cha Fogarty, kama sehemu ya Taasisi za Afya za Kitaifa za Marekani, imejitolea kwenye afya ya ulimwengu, ambayo inakusudia kuboresha ustawi na kufikia usawa wa huduma za afya kwa watu wote duniani. Kazi ya Fogarty inajumuisha kuandaa kizazi kijacho cha wanasayansi kujibu vitisho vya sasa na vya baadaye vya magonjwa. Kituo hiki kinatoa mafunzo, kinawezesha ushirikiano kati ya watafiti, na kinasaidia tafiti za afya zinazotegemewa katika nchi za kipato cha chini na cha kati.

Fogarty inafadhili zaidi ya miradi 500 inayohusisha takribani vyuo vikuu 100 vya Marekani. Fogarty pia inakusanya akili bora za kisayansi kushughulikia matatizo muhimu ya utafiti wa afya ulimwenguni kama vile mwitikio wa janga, upinzani dhidi ya dawa za kuzuia au kuua vimelea vya maradhi na kuimarisha uwezo wa utafiti katika nchi washirika.

**Kwa ufupi, Fogarty huwekeza katika watu—watafiti wa afya—ambao huendeleza utaalamu wa kisayansi katika nchi zilizo na ufikiaji mdogo wa mafunzo ya utafiti wa afya.**

Katika karne ya 21, utafiti wa afya unazidi kuwa mgumu, unaohitaji jitihada za pamoja kati ya watafiti wenye uzoefu na utaalamu mbalimbali. Magonjwa mengi muhimu hayawezi kuchunguzwa nchini Marekani pekee, wakati mengine yanaweza kuchunguzwa vizuri zaidi nje ya nchi ambapo yameenea zaidi. Ili kutatua matatizo ya afya ya kimataifa, zinahitajika timu za kimataifa ambazo ni nyeti kwa tamaduni na jamii. Jukumu la Fogarty ni kusaidia kujenga ushirikiano huu wa kisayansi, utakaopelekea ugunduzi ambao utawafaidisha wote.

**Zaidi ya wanasayansi 6,000, duniani kote, wamepokea mafunzo muhimu ya utafiti kupitia Fogarty tangu kuanzishwa kwake mnamo mwaka 1968.**

## Programu za utafiti na mafunzo ya Fogarty

- Magonjwa Sugu, Yasiyoambukiza na Matatizo Katika Maisha Yote
- Ikolojia na Mageuzi ya Magonjwa ya Kuambukiza
- Utafiti wa Matatizo ya Ubongo na Mfumo wa Neva Ulimwenguni katika kipindi chote cha Maisha
- Afya ya Mazingira na Kazi Ulimwenguni
- Mafunzo ya Utafiti wa Magonjwa ya Kuambukiza Ulimwenguni
- Kuunganisha Sayansi ya Takwimu kwa Ugunduzi na Ubunifu wa Afya barani Afrika
- VVU/UKIMWI
  - Mafunzo ya Utafiti wa VVU
  - Utafiti wa Magonjwa Yasiyoambukizwa yanayohusiana na VVU katika Taasisi za Nchi zenye kipato cha Chini na cha Kati
  - Kupunguza Unyanyapaa ili Kuboresha Kuzuia VVU/UKIMWI, Matibabu na Huduma kwenye Nchi zenye Kipato cha Chini na cha Kati
- Teknolojia ya Afya kwenye Rununu na Matokeo
- Utafiti wa Tumbaku na Afya na Kujenga Uwezo
- Mafunzo ya Utafiti wa Matukio yanayoathiri akili na Majeraha

Fogarty inaunganisha masomo ya usambazaji na utafiti wa utekelezaji kupitia programu zake zote, kwa sababu ugunduzi wa kisayansi una athari tu wakati unawafikia watu na kuboresha maisha. Mnamo mwaka 2016, Kituo cha Fogarty cha Mafunzo ya Afya ya Kimataifa kilizindua Zana za Sayansi ya Utekelezaji ambayo hutoa mifano, mifumo, mikakati, na mbinu zilizofanikiwa kusaidia wanasayansi kutafsiri kazi zao katika sera na matumizi. Zana hii inaendelea kuwa na wastani wa kuonekana kwa kurasa 1,800 kwa mwezi.

## Fogarty huendeleza viongozi

Mpango wa Afya wa Kimataifa wa Fogarty kwa Washirika na Wanafunzi umetoa msaada kwa mafunzo ya utafiti wa kliniki kwa zaidi ya washirika 800 (wanafunzi wa baada ya uzamivu na Uzamili) na wanafunzi 650 (wanafunzi wa sasa wa Uzamivu na Uzamili) katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Mwaka 2022, mpango huo ulibadilishwa jina na kuitwa UZINDUZI (Uzinduzi wa Viongozi wa Baadaye katika Mafunzo ya Utafiti wa Afya ya Kimataifa) na kupanuliwa ili kuhamasisha ushiriki wa watu binafsi kutoka idadi duni ya watu wa Marekani.

Wakati wanasayansi waliofundishwa na Fogarty wanapofanya majukumu muhimu katika nchi zingine, ushawishi wa Marekani unapanuliwa kote ulimwenguni. Wanafunzi wengi wa Fogarty wameendelea kuwa viongozi wa afya ulimwenguni. Majukumu ya uongozi wa zamani na wa sasa yaliyoshikiliwa na wanafunzi wa zamani ni pamoja na: Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Uganda, Waziri wa Afya wa Peru, Mkuu wa magonjwa ya kuambukiza wa Shirika la Afya la Marekani chini ya Shirika la Afya la Dunia (WHO) na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Utafiti wa Matibabu la India.

## Fursa za kipekee za utafiti zinaweza kuharakisha ugunduzi

Umuhimu wa kuzuia ugonjwa wa Alzheimers unaweza kuwa katika kujifunza familia pana na ugonjwa wa Alzheimers wa kurithi, wa mapema huko Kolombia vijijini. Fogarty imetoa mafunzo muhimu ya kisayansi ili watafiti wa ndani wa Kolombia waweze kufanya uchunguzi wa ubongo, uchambuzi wa vinasaba na mbinu zingine za kisasa. Kazi yao tayari imewezesha jaribio la kliniki la dawa iliyotengenezwa nchini Marekani ambayo inaweza kusaidia kukomesha Alzheimers katika hatua yake ya kwanza.

Mfano mwingine unatoka vijijini Brazil ambapo wanasayansi waliofunzwa na Fogarty kuchunguza ugonjwa wa Chagas walielekeza ujuzi wao wa utafiti ili kuchunguza Zika wakati mlipuko ulipoanza mnamo 2015. Maambukizi ya Zika, ambayo kimsingi huambukizwa na kuumwa na mbu, kwa ujumla ni kidogo, lakini yale yanayotokea wakati wa ujauzito yanaweza kusababisha kasoro katika kuzaliwa, pamoja na kichwa cha mtoto mchanga kuwa kidogo, aina ya matatizo ya neva.

Kama janga la UVIKO-19 lilivyotufundisha, magonjwa hayaheshimu mipaka au kutii ratiba. Kwa kuzuia milipuko pale inapotokea, tuna uwezekano mkubwa wa kuizuia isienee katika mataifa na ulimwenguni kote. Mipango ya Fogarty inalenga kuhakikisha kuna wafanyakazi wa ndani na miundombinu ya ndani iliyopo, katika mazingira yote, tayari kugundua magonjwa ya mlipuko wakati wa kuanza kwake na yenye uwezo wa kuzuia mlipuko, na hivyo kupunguza athari za magonjwa.

**Wafadhili na wanafunzi wa Fogarty walichukua jukumu kubwa katika kukabiliana na UVIKO-19 katika utafiti katika nchi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na China, Haiti, Peru, na Afrika Kusini.**

Mnufaika wa zamani wa Fogarty Dkt. Christian Happi wa Nigeria alikuwa wa kwanza kupanga genomu kamili ya virusi vya UVIKO-19 barani Afrika wakati Dkt. Sikhulile Moyo Mwenzake wa zamani kutoka Botswana alikuwa wa kwanza kugundua Omicron anuwai. Dk. Andrew Kambugu, aliyepata mafunzo ya hali ya juu katika utafiti wa magonjwa ya kuambukiza nchini Marekani kwa msaada wa Fogarty, alianzisha mpango wa kimataifa wa usalama wa afya katika Taasisi ya Magonjwa ya Kuambukiza ya Uganda mnamo 2016. Baadaye, hii ilimwezesha kuchangia katika kukabiliana na UVIKO-19 kwa taifa lake. Wakati huo huo, ndani, Idara ya Fogarty ya Epidemiolojia ya Kimataifa na Mafunzo ya Idadi ya Watu inaendelea kusaidia utayarishaji wa janga kupitia utafiti wake unaoendelea pamoja na mafunzo na zana zinazotoa katika maeneo ya mfano wa magonjwa na magonjwa ya jeni.



### Ungana na Fogarty

Tovuti: www.fic.nih.gov
Jisajili: go.nih.gov/SubscribeFogarty